



TENGENZEZA BLOG

Prosper Mtabo

KUHUSU MWANDISHI

Prosper Mtabo ni mwandishi wa vitabu kuhusu masuala ya mtandao sana sana kuhusu tovuti kwa ujumla. Vile vile ni mshauri na mtaalamu wa search engine optimisations(seo).

**Kwa ushauri, msaada au huduma tumia
email: prospermtabo@gmail.com
phone: 0765696086**



Kuanzisha tovuti/blog ni moja ya kazi zinazoshika kasi siku hadi siku. Kabla ya kuanzisha blog/tovuti ni lazima uwe na wazo muhimu litakalokuwezesha kudumu katika kazi hii ya uendeshaji wa blog/tovuti. Idadi kubwa ya watu wanaingia kwenye fani hii ya blogging bila kuwa na malengo hatimaye wanaziacha blog zao. Wengine wanaingia kwa msukumo kwa kusikia kuwa blogging inaingiza pesa.

Lakini pamoja na hayo yote hayo, unaweza kuitumia blog yako kujiajiri wewe mwenyewe. Kitu cha msingi ni kuwa ukifanikiwa kupata watembeleaji wa kutosha basi kuna uwezekano wa blog yako kuanza kukuingizia kipato.





Kwanza kabisa ni kwamba kazi hii ya blogging siyo rahisi kama watu wanavyofikiria.

Blogging inahitaji muda wako na uvumilivu sana.

Muda mwingine itakubidi uingie gharama kuweza kuiendesha blog yako.

Kama yaliyotajwa hapo juu unayaweza basi endelea kusoma kitabu hiki, kama huyawezi basi nivyema ukakinga kitabu hiki.





**kitu cha kwanza kabisa uwe na wazo la blog yako.
Je hiyo blog inahusu nini?
Je ni kwa ajili ya biashara?
Unawezaje kupata contents za blog yako?
Walengwa ni akina nani?**

Lazima uweze kuwa na lengo la blog yako .maana hauwezi ukafungua blog bila kuwa na wazo ambalo utaliandika. Blog yako inaweza kujumuisha vitu vingi. Inaweza kuhusu habari(makala),vitu unavyovipenda, biashara yako, au kitu chochote ambacho ungependa watu wasikie kutoka kwako.






Kitu cha pili ni kujua hiyo blog yako itatoa taarifa gani au kuwasaidiaje watu. Kama unaandika kitu fulani lazima kiakisi maisha au kiguse mada itakayoweza tovuti yako kusomwa. blogging ni kwa ajili ya kutoa taarifa na msaada kwa watu. Andika posts zitakazovutia watu kusoma. Ukiandika posts ambazo hazina mvuto huwezi kupata watu wa kusoma na utakosa watembeleaji.

Kitu kingine ni kuangalia blog ambazo zinaandika mada ambazo unataka kuziandika. Hii itakusaidia kuapata uzoefu na kujua jinsi gani ya kuandika posts. Utajua mtiririko na jinsi wanavyoandika. Utajua posts nyingine ambazo ungependa nawe kuziandika. Epuka ku-copy na ku-paste maudhui ya watu wengine.





Kitu cha tatu je ni sehemu gani ungependa kuhost blog yako. Ili kuweza kutumia blog yako inakubidi uwe na sehemu ambayo utaiweka. Kuna njia mbili ambazo unaweza kuzitumia.

moja ni kutumia blogging platform ambazo ni bure kabisa kama za *blogger(blogger.com)* na *wordpress(wordpress.com)*. Ukituma blogger jina lako litakuwa *jinalako.blogspot.com* ukitumia wordpress jina lako litakuwa *jinalako.wordpress.com* Hizi njia ni bure kabisa,

Vile vile unaweza kutumia custom domains yaani kutumia *yourdomain.com/co.tz/net* kwenda katika blogger au wordpress. Ambapo hii njia wanatumia bloggers wengi sana kwa sasa.

Njia ya pili ni kuhost blog yako mwenyewe hapa itakubidi ununue domain name na hosting (uwe na kianzio pesa angalau TSH.100000(kila mwaka) ukitoa web design). Hii njia ya pili unaweza kutumia content management systems kama wordpress(*wordpress.org*), drupal na joomla. Kitabu cha kuweza Kutengeneza blog kupitia content management system ya wordpress(*wordpress.org*) kinapatikana kwa TSH.5000/= tu (pdf).






Kitu cha mwisho kabisa ni njia za kuitangaza blog yako. Je unatumia njia zipi za kutangaza blog yako. Hapa ndipo watu wengi wanapokwama.

Bila ya kuitangaza blog yako hautoweza kupata watembeleaji wowote. Lazima utumie mitandao ya kijamii katika kutangaza blog yako. Lazima blog yako iwe na maudhui ambayo mtu yoyote atapenda kuyasoma muda wowote (sio habari za udaku). Lazima uandike posts mara kwa mara ambazo zina ubora wa kutosha. Lazima uelimishe jamii.

Ili kuweza kuwatosheleza watembeleaji wako. Epuka ku-copy na ku-paste maudhui kutoka blog nyingine kwenda katika blog yako maana si njia nzuri ya kufanya blogging.



MWISHO



KUENDELEA KUPATA VITABU
VYANGU VYA BURE KUHUSU
BLOGGING KILA WIKI TUMA
NENO "BLOGGING" KWENDA
prospermtabo@gmail.com